


KUTOKA KATIKA KITUO CHA UTAFITI NA UBUNIFU WA MAENDELEO YA SERIKALI MTANDAO (eGOVRIDC)

FAHAMU KUHUSU ChatAI

Akili Bandia maarufu kama '**Artificial Intelligence (AI)**' ni teknolojia inayolenga kujenga mifumo ya kompyuta inayoweza kufanya kazi kwa kufanana na akili ya binadamu.

Teknolojia hii, ni mionganini mwa teknolojia mpya zinazoibuka kwa sasa duniani na kushika kasi ya matumizi kwenye sekta mbalimbali, zikiwemo sekta za biashara, afya, elimu n.k. Lengo la teknolojia hii ni kutoa uwezo wa kufikiri, kujifunza, kutatua matatizo, na kufanya maamuzi kwa njia inayofanana sawa na ubongo wa binadamu.

Programu za AI zinaweza kufundishwa kutambua vitu kama picha au sauti, hii inaweza kutumika katika maeneo kama utambuzi wa vitu, sura, maandiko au hotuba, Mfumo unaotumia AI pia inaweza kufundishwa kuelewa na kutoa majibu kwa lugha ya asili, kama vile mazungumzo ya binadamu.



Sasa nakupa habari njema rafiki! Kituo cha Utafiti na Ubunifu cha Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGOVRIDC), kimebuni na kujenga programu ya kompyuta ya Akili Bandia au Artificial Intelligence iitwayo ChatAI (Chat AI), inayoweza kuwasiliana na binadamu kupitia ujumbe wa maandishi au sauti na kutoa habari au msaada kulingana na kile ambacho mtumiaji anasema au kuandika.

Subiri sasa nikusimulie vizuri, program hii imewezeshwa kutumia lugha yetu pendwa ya taifa yaani Kiswahili, hivyo usiwe na wasiwasi kila Mtanzania anapaswa kufurahia na kutumia hivyo, kazi ni kwako sasa. Pia ChatAI inaweza kupokea Sauti au maandishi nayo ikakujuza kwa sauti au maandishi yaani (*Text to Speech and Speech to Text*)

Unajiuliza ChatAI huyu anafanyaje kazi? Ni rahisi sana hebu fikiria kama msaidizi wa kawaida wa dijiti ambaye unaweza kuchati naye, kama vile unavyotuma ujumbe kwa rafiki, lakini rafiki huyu wa dijiti amefanyiwa programu ya kutoa habari za Serikali na kusaidia katika kazi za usaidizi kwa wateja.

Ahaa! Umeelewa sasa eeh! Lengo kuu la program hii ni kufanya huduma za Serikali ziweze kupatikana zaidi na rafiki kwa watumiaji, na hapa ile dhamira ya Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) ya kusimamia matumizi ya TEHAMA Serikalini ili kuhakikisha huduma za Serikali zinawafikia wananchi mahali walipo inatimia kupitia ChatAI huyu.

Kingine muhimu unapaswa kujua ni kuwa; ChatAI huyu anaweza kueleza huduma mbalimbali za Serikali na kujibu maswali ambayo watu wanaweza kuwa nayo kuhusu huduma hizo. Hii inamanufaa kwa raia ambao wanataka kuelewa huduma zinazotolewa na Serikali lakini hawajui mahali pa kupata habari sahihi na sasa ChatAI huyu anakujibu maswali yote.

Si hivyo tu rafiki,nikujuze sasa; ChatAI hii inaweza pia kubadilisha ujumbe wa maandishi kuwa sauti, hapa namaanisha kuwa inaweza kusoma majibu kwa watumiaji, kwa sauti kwa watu ambao wanapendelea kusikiliza badala ya kusoma (*Text to Speech and Speech to Text*).

Umeona ee sasa! ChatAI ni msaidizi wa dijiti wa habari za Serikali na yupo tayari kwa watumiaji, wenye uwezo wa kusiliana kupitia maandishi na hata kubadilisha maandishi kuwa sauti kwa urahisi zaidi.

Kwa taarifa zaidi tembelea www.ubunifu.ega.go.tz